# ***May Swahili translation.***

## ***Ni gharama gani unaweza lipa kuona injili ikienda mbele?***

Zamani za kale katika nchi ya mbali, yule mfalme mwenye nguvu zaidi na mali zaidi duniani alisikia rohoni mwake akiwa na shauku la kueneza ujumbe mwema wa upendo wake kwa watu wa dunia. Akaamua kutuma kitu chake cha dhamana zaidi, Mwana Wake. Alijua ingalikuwa hatari, lakini shauku lake la kuwafikia wanadamu likamshinda. Ilimgharimu Mungu mwanawe kuokoa nafsi yako.

Miaka kadhaa iliyopita mimi na mwana wangu wakiume tulikuwa tukipeana Bibilia kule Uchina. Usiku mmoja kabla tutoke tuelekee misheni yetu, nikaota kuwa mwana wangu alienda kwa misheni yake na akakosa kurejea. Kutokana na ndoto hii, nikamwambia mwanangu kuwa hataenda. Mwanangu pia akanieleza hata yeye aliota. Katika ndoto lake, alijua kwamba akiyatenda yote niliyomweleza atende, atakuwa salama. Baada ya yeye kuniambia ndoto yake, mwanangu akanikumbatia, na kwa ujasiri lakini kwa upole, akaninong'onezea huku akilia, ' baba, ni gharama gani unaweza lipa kuona injili ikienda mbele?' kisha akaingia kwa gari la moshi na kuanza safari yake.

*Ombi la leo*

Baba, najua unanipenda na una kila mpango kuhusu maisha yangu. Naomba unipe nguvu niinuke zaidi ya hofu zangu na nifanye mapenzi Yako bila kujalisha gharama. Nahesabu kuwa fursa, kuitwa kukutumikia Wewe. Kwa hivyo, najinyima mimi, nachukua msalaba wangu, na ninakufuata.

*Maandiko ya leo*

Mathayo Mtakatifu 13:46; Alipopata lulu moja ya thamani kubwa, alienda akauza yote aliyokuwa nayo, akainunua lulu ile.

1 Wakorinitho 6:20; Mlinunuliwa kwa bei kubwa. Kwa hiyo, itumieni miili yenu kwa ajili ya kumtukuza Mungu.

***Uinjilisti ni mbio za kushindana na wakati.***

Wenye dhambi hawazaliwi kila siku na kila mmoja wetu ana fursa moja yakutimiliza mapenzi ya Mungu na makusudio yake kuhusu maisha yetu. Kabla tufikie hiyo nyumba ya kiusemi ya mwisho wa barabara, lazima kwanza tufikie kila nyumba nyingine yoyote hapa duniani. Uinjilisti wa dunia nzima waweza timizika tu kwa kizazi kimoja. Hauwezi kuendeleshwa kwa kizazi kingine.

Mungu hana wajukuu. Ana wana pekee na kila mtu ana siku kadhaa ambazo ataokoka, akuwe ndani ya Kristo, na afanyike mfanyi kazi mwenye mazao katika mavuno ya nafsi kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Hii ni siku yako, huu ni wakati wako, haya ni maisha yako. Uinjilisti ni mbio za kushindana na wakati.

*Ombi la leo*
Mpenzi Bwana, nipe huruma za wale wamepotea na unisaidie kutazamia maisha yangu katika mapenzi Yake kwa ajili ya kizazi changu. Nifunze kufanyika mvuvi wa watu na unipe hekima ua kushinda nafsi kwa ajili ya ufalme Wako.

*Maandiko ya leo*

2 Wakorintho 6:2; Mungu asema hivi: "Wakati wa kufaa nimekusikiliza, wakati wa wokovu nikakusaidia." Basi, sasa ndio wakati wa kufaa, sasa ndiyo siku ya wokovu!

Waefeso 5:15-17; Basi, muwe waangalifu jinsi mnavyoishi: Msiishi kama wapumbavu, bali kama wenye hekima. Tumieni vizuri muda mlio nao maana siku hizi ni mbaya. Kwa hiyo, msiwe wapumbavu, bali jaribuni kujua matakwa ya Bwana.

## *Ongea lugha ya wanao kusikiliza*

Mtume Paulo alisema kwamba afadhali anene maneno matano ambayo wanao sikiliza wataelewa kuliko maneno elfu moja wasio weza kuelewa. Haya ni mambo mimi kuweka maanani ninapopata nafasi yakunenea watu wengine kuhusu kanuni za Neno la Mungu. Neno la Mungu haliwezi kubadilika, lakini jinsi tunavyowasilisha Neno la Mung ni uamuzi wetu.

Tilia maanani unaye mnenea na uhakikishe unawasiliana na wale wanao kusikiliza kwa lugha wanayoielewa. Kama ni watu wa umri fulani, vikundi vya jinsia fulani, ama tamaduni mbali mbali ama imani mbali

mbali ,chagua maneno yako kwa umakini uhakikishe umetumia fursa yako vilivyo. Nena lugha ya wanao kusikiliza.

*Ombi la leo*

Mpenzi Mungu, nisaidie nitumie fursa yoyote nitayopata leo vyema iwezekanavyo kwa kwanza kutilia manani ninayemnenea na jinsi naweza kuwafanya wanielewe. Nipe neema ya kushiriki Neno Lako na wengine kwa njia inayoweza kubadilisha maisha yao. Amina

*Maandiko ya leo*

1 wakorintho 9:19-23; Kwa hiyo, ingawa mimi si mtumwa wa mtu yeyote, nimejifanya mtumwa wa kila mtu ili nimpatie Kristo watu wengi iwezekanavyo. Kwa Wayahudi nimeishi kama Myahudi ili niwapate Wayahudi; yaani, ingawa mimi siko chini ya Sheria, nimejiweka chini ya Sheria kwao, ili niwapate hao walio chini ya Sheria. Na kwa wale walio nje ya Sheria, naishi kama wao, nje ya Sheria, ili niwapate hao walio nje ya Sheria. Hii haimaanishi kwamba mimi niko nje ya sheria ya Mungu, maana nabanwa na sheria ya Kristo. Kwao walio dhaifu nimejifanya dhaifu ili niwapate hao walio dhaifu. Nimejifanya kila kitu kwa wote ili nipate kuwaokoa baadhi yao kwa kila njia. Nafanya haya yote kwa ajili ya Habari Njema, nipate kushiriki baraka zake.

## *Kila barabara huelekea pahali*

Sisi huchagua barabara tunayoipitia kwa sababu tofauti…. Barabara tunayoichagua itatuelekeza pale tunapotaka kuenda. Kila barabara, huelekea pahali. Mwisho wake sana sana waweza kubashirika, hasa kama tuna ramani ama tumeelekezwa na wengine wanao ifahamu barabara hii. Nadra, tunaweza kunug'unika tunapofika mwisho wa barabara yenye kubashirika ya safari yetu. Barabara za maisha yetu sio tofauti. Neno la Mungu linatupea ramani na wahuduma wake mara nyingi hutupa mwelekeo ili tujue nini tutapata hapo mbele ya bara bara ambayo tumeichagua.

Unaelekea wapi? Uko kwa barabara itakayo kuletea uhusiano mzuri, ndoa iliyo imarika na jamii, ubora wa siku za usoni i? Kama sivyo kuna uamuzi mmoja tubu….

*Ombi la leo*

Baba, nakushukuru kwa kuumba hatima inayoeleweka kwa maisha yangu. Nifunze kuifuata ramani na mwelekeo unaonipa Wewe. Nisaidie

kutia maanani kila chaguo na inapoelekea. Nisaidie pia, kupeana mweleko wa kiungu kwa wengine.

*Maandiko ya leo*

Mithali 16:17; barabara kuu ya waliosimama ni kuachana na uovu; anayhifadhi mapito yake huokoa nafsi yake.

Mithali 22:3; mwenye busara huyaona mabaya na kujificha; bali wajinga huendelea mbele na kuumia.

Isaya 55:9; kwa maana kama mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi ; kadhalika njia zangu ziko juu sana kuliko njia zenu na mawazo yangu yako juu sana kuliko mawazo yenu.

## ***Sio kile unachopitia ila ni pale unapoelekea.***

Kila barabara inaelekea mahali. Katika safari yako kutoka ulipo sasa hadi unapotaka kuenda, mara kwa mara tunalazimishwa ***kupitia*** mambo ambayo hatuyafurahii ili ***tufikie*** yale tutafurahia. Katika nyakati hizi, twahitaji kujikumbusha kuwa sio yale tunapitia lakini ni pale tunapoelekea panapojalisha sana.

Mfano, mmoja aweza kutamani kuwa na elimu ya juu na amalize kwa kufanyika daktari wa matibabu. Kama hii ndiyo hatima yao na barabara wanayoweza kuchagua kupitia. Kwenye barabara yakufanyika daktari, lazima wapitia vipindi vya mafunzo, miaka ya elimu, na , bila shaka, muda mwingi wa kuchoka na kuishiwa na nguvu na hata labda kugandamizwa. Hata hivyo, kama mtu hajaamua kupitia mambo haya asiyo yafurahia ili apate yale ambayo atayafurahia, waweza kosa kufurahia maisha kamwe.

*Ombi la leo*

Baba wa mbinguni, fungua macho ya kuelewa kwangu ili nijue tumaini ya wito wangu ndani Yako. Nataka kutazamia pale ninapoelekea sio pale nilipo sasa. Tafadhali nisaidie kuamini na kutarajia Kwako ili niweze kufikia furaha na amani iliyotimilika sasa. Ahsante!

*Maandiko ya leo*

1 wakorinitho 4:17-18; Ndiyo maana nimemtuma Timetheo kwenu. Yeye ni mtoto wangu mpenzi na mwaminifu katika Bwana. Atawakumbusheni njia ninayofuata katika kuishi maisha ya Kikristo; njia ninayofundisha

kila mahali katika makanisa yote. Baadhi yenu wameanza kuwa na majivuno wakidhani kwamba sitakuja tena kwenu.

Mithali 29:18; pasipo maono, watu huacha kujizuia; bali ana heri mtu yule ahikaye sheria.

## ***Hutawahi kufaulu kumuongoza mtu ambaye hutaki kuachilia***

Ufalme wa Mungu umeundwa ufanye kazi kama vile tunatazama katika majeshi yetu. Kuna wakubwa na wadogo, watawala, masharti, na kazi ambazo zinajulikana. Majeshi yanampangilio unaolazimisha kila mtu ajitokeze  na atende kile ameambiwa atende. Wakati mwingine wanaambiwa wao ndio wakusimamia na wakati mwingine  wanajikuta wameambiwa wawafuate wengine walio kwenye usimamizi… yote haya ni muhimu na yanakubalika ili kila jukumu litimizwe.

Viongozi ambao hawana ujasiri na hawataki kupeana amri kwa kuogopa wafuasi wao waweza kosa kuzitii, waweza kuwa hawongezi hata kidogo. Hawa viongozi wanafuata maono ambayo yanapendeza watu  ama sauti ambazo zina sikika sana zinazokubali kila mtu atende kilicho sawa machoni mwake mwenyewe. Hii sio njia ya Kifalme. Ukipewa nafasi ya kuongoza, kuwa mpole, mwenye huruma, na uchukue ushauri… lakini uongoze kwa ushawishi wako mwenyewe, ukikumbuka hautawahi weza kuwaongoza wale ambao hawataki kuwachilia.

### *Ombi la leo*

Baba, tafadhali nisaidie kuwa kiongozi kama Yesu;mtu aliye na ujasiri kwa kile ulichomwita atende. Sitatingizwa na tisho la kumpoteza mtu. Nahitaji nguvu zako na hekima Yako ili kuwasilisha mwelekeo wangu kwa njia ya upole.

### *Maandiko ya leo*

Matendo ya Mitume 15:37-41; Barnaba alitaka wamchukue pia Yohane aitwaye Marko. Lakini Paulo hakupendelea kumchukua Marko, ambaye awali aliwaacha kule Pamfulia na kukataa kushiriki katika kazi yao. Basi kukatokea ubishi mkali kati yao, na wakaachana. Barnaba akamchukua

Marko, wakapanda meli kwenda Kupro. Naye Paulo akamchagua Sila, na baada ya ndugu wa mahali hapo kumweka chini ya ulinzi wa neema ya Bwana, akaondoka. Katika safari hiyo alipitia Siria na Kilikia akiyaimarisha makanisa.

## *Kitu kilicho anzilishwa kwa makosa hakitarekebishwa na wakati*

Kama mtu atajenga nyumba na msingi ukose kuwa imara, hatimaye nyumba nzima itaanguka chini. Kama uongezi wa chama Fulani cha kisiasa una ufisadi, wakati huufanya uwe mbaya zaidi. Mambo mabaya yakiachiliwa hufanyika mabaya zaidi.

Makanisa mengine mapya yameanzishwa na watu ambao wamekuwa sababu ya kutengana kwa kusanyiko walilokuwa washirika mbeleni. Kama kazi hizi zinapandwa na mbegu ya uasi, basi bila kujalisha kanisa litachukua mwelekeo upi usoni, litaendelea kuwa na matatizo na litapitia mgawanyiko kama tunda la mizizi yake. Suluhisho la kipekee ambalo laweza kupatikana laweza kuwa kuomba msamaha wa Mungu ambaye aweza geuza madoa ya chui na afanye upya kutokana na uzee. Kanuni za maisha yetu ya kila siku hazina utofauti: chochote kinacho anza kima kosa, hakitarekebishwa na wakati.

### *Ombi la leo*

Baba, nionyeshe mambo ambayo nimeanza na makosa. Nataka kutubu na nikuweke Wewe  katika mizizi ya yote nitendayo. Najua unaweza kunisaidia nianze tena. Nisamehe mahali nimekukosea na uunde ndani yangu njia mpya inayoishi.

### *Maandiko ya leo*

Mathayo Mtakatifu 3:10 Basi, shoka liko tayari kuikata mizizi ya miti; hivyo, kila mti usiozaa matunda mazuri, utakatwa na kutupwa motoni.

Mathayo Mtakatifu 6:22-23 "Jicho ni taa ya mwili. Kama jicho lako ni zima, mwili wako wote utakuwa katika mwanga. Lakini ikiwa jicho lako ni bovu, mwili wako wote utakuwa katika giza. Basi, ikiwa mwanga ulioko ndani yako ni giza, basi, hilo ni giza la kutisha mno.

## *Mto hauwezi ukainuka zaidi ya kiwango cha kina chake*

Maji huteremka chini ya mlima. Hii ni kanuni ya sheria ya Mungu unao dhihirisha ukweli unaofunika  sio ulimwengu wa kiasili pekee ila pia wa kiroho. Sisi sote tunachagua mwanzo wetu wa maisha, nguvu, na fanaka. Wengine huchagua pesa na wengine huchagua walezi.  Chaguzi hizi zote zaweza kuwa na manufaa na mara nyingi zinachangia vizuri fanaka yetu. Hata hivyo zote mbili hazihitimu kuwa mwanzo wetu.

Mto hauwezi kuinuka zaidi ya kina chake na pia mwandamu. utawekewa kiwango Kamwe na viwango vyaa mwanzo wako. Kwa nini ujenge maisha yanayo wekewa kiwango na vile pesa, mamlaka, ama uweza  waweza kukufanyia.  Toa viwango hizo kwa kumchagua Mungu kama chanzo chako kimoja cha ukweli na uruhusu wengine wachangie vile Mungu anataka.

*Ombi la leo*

Baba, ahsante kwamba nina chanzo ndani yangu ambacho sitakikwaza. Ahsante kwa Roho Mtakatifu anayekuwa ndani yangu kila siku. Nionyeshe kile kinahitajika kubadilishwa maishani mwangu ili nisizuie chanzo. Wacha mto wako utiririke ndani yangu na umwagike kutoka kwangu.

*Maandiko ya leo*

Yohana 7:38 Kama yasemavyo Maandiko Matakatifu: `Anayeniamini mimi, mito ya maji yenye uzima itatiririka kutoka moyoni mwake!"`

1 Timotheo 6:17 Waamuru watu walio matajiri katika mambo ya maisha ya sasa, wasijivune, wasiweke tumaini lao katika mali isiyoweza kutegemewa; bali wamtegemee Mungu, ambaye kwa ukarimu hutupatia vitu vyote tuvifurahie.

## ***Simama uonekane, nena usikike lakini keti chini utambulike***

Huu ni ushauri msichana mdogo alipewa na babu yake akitarajia itamuadaa kuishi maisha yakumpendeza Mungu na kupewa kibali na wanadamu. Kanuni za Neno la Mungu ni rahisi lakini za kumaanisha. Lazima tuchukue msimamo ili wengine waona kwa uwazi upendo wetu na ushawishi wetu maishani. Lazima pia tunene ili tusikike hasa kwa wale  wanaohitaji mwelekeo dhabiti. Sauti yetu yaweza kuwa tochi ya mwangaza kwa wale walio kwa giza  na chanzo cha mwelekeo kwa nafsi inayoumia.

Twafaa kusimama tuonekane, tunene ili tusikike, lakini tuketi chini ili tuthaminiwe.mbingu na dunia zote huwakataa wenye kiburi na majivuno. Kwa hivyo twafaa kujinyenyekeza chini ya mkono Mkuu wa Mungu ili tuweze kuinuliwa  na Yeye pekee kwa wakati wake.

*Ombi la leo*

Baba, naomba unipe ujasiri wa kusimama unaponielekeza. Nipe maneno yakufanya utofauti na hekima, iliyolainishwa na unyenyekevu, kuwa mtulivu kwa wakati unao faa. Nataka kuwa mwangalifu kwa hali ambazo umeniweka ndani yake ili niwe chombo Chako cha kubariki wengine.

*Maandiko ya leo*

Mithali 17:27 azuiye maneno yake ni mwenye maarifa; na mwenye roho ya utulivu ana busara.

## *Unaandika hadithi watakayosema wengine kukuhusu wewe*

Kila maisha ya mtu hufanyika hadithi. Kama mtume Petro, hata wewe utajulikana milele  na kile wengine watakumbuka kukuhusu wewe.uamuzi mbaya, uamuzi usio faa, na hata makosa yenye gharama yafaa kutazamwa kama utaratibu wa maisha  na sio kuruhusiwa kutufanya tuache kurekebisha makosa yetu na kuandika sura mpya ya siku zetu za usoni. Hadithi ya maisha ya Petero haikumaliza na yeye akimukana Yesu na wala ya mfalme Daudi kuisha na yeye akiamuru rafiki yake auwawe.

Kama vile ilikuwa na watu wengi wa Bibilia ba majemedari wa kale, maisha yake hayafai kuisha na uamuzi wako mbaya. Peana siku zako za usoni kwa Mungu leo. Wacha ya kale yawe kale na uanze kuandika sura mpya ya maisha.

*Ombi la leo*

Baba, ahsante kwa kunipea maono na mtazamo wa siku zangu za usoni. Nataka maisha yangu yawe andiko ambalo Wewe tu ndiye waweza kuandika. Nipe neema niwe kielekezo cha mapenzi  Yako  na unipeleke kwa siku yangu kuu zaidi.

*Maandiko ya leo*

Mithali 22:1 heri kuchagua jina njema kuliko mali nyingi; na neema kuliko fedha na dhahabu.

Muhubiri 7:1; heri sifa njema kuliko marhamu nzuri; na siku ya kufa kuliko siku ya kuzaliwa.

Mithali 13:22; mtu mwema huwaachia wana wa wanawe uridhi; na mali ya mkosaji huwa akiba kwa wenye haki.

## *Ni ukweli unaohuzunisha, lakini wakati mwingine kuwachana na mtu kutasababisha kuachana na shida.*

Umewahi katika mchezo na mchezaji mmoja akawa akifanya kosa baada ya lingine kwamba kama wangekosa kubadilika ingesababisha kukosa kikombe? Kisha mchezaji mpya akingia  kufanya kazi ya yule na hatimaye mambo yakawa bora zaidi?  Kuna mtu ofisini mwako ambaye anasababisha matatizo kila siku?  Kuna mtu maishani mwako ambaye kila siku ukiongea na yeye anaongea kuhusu matatizo? Je, ni wewe mtu huyu?

Yona 1:12; ‘ na akawaambia, nichukue na mnitupe ndani ya bahari; nayo bahari itakuwa tulivu kwenu: kwa maana ninajua ni kwa sababu yangu mawimbi haya yamewachafukia.’ Ni vizuri kuwa Yona aligundua kuwa yeye ndiye alikuwa kiini cha matatizo. Badilika leo. Tupa ukale wako mbali na uanze upya. Ni siku mpya kabisa na ina fursa zisizokuwa na kikomo. Ni ukweli wenye kuhuzunisha, lakini wakati mwingine kumuacha huyo mtu itafanya shainda ziishe.

*Ombi la leo*

Baba, tafadhali nisaidie kuwa suluhisho wala sio shida. Nisaidie kuwa jawabu sio swali. Mimi ni sehemu ya kitu kikubwa sana, nifanye niwe mkubwa kwa makusudi Yako… katika uhusiano wangu na Wewe, katika jamii yangu, na kazi yangu.

*Maandiko ya leo*

1 Samueli 12:14;kama mkimcha Bwana na kumtumikia, na kuisikiza sauti Yake, msiasi amri ya Bwana tena kama ninyi na mfalme anayewatawala; mkimfuata Bwana Mungu wenu vyema.

Warumi 8:3 Mungu ametekeleza jambo lile ambalo Sheria haikuweza kutekeleza kwa sababu ya udhaifu w binadamu. Mungu alimtuma Mwanae akiwa mwenye mwili sawa na miili yetu sisi wenye dhambi, ili aikabili dhambi, na kwa mwili huo akaiangamiza dhambi.

## *Kushiriki hekima bila unyenyekevu na neema kutaweza kuleta chuki...hata wakati uko sahihi.*

Watu wanaokuwa sahihi kila wakati huwa hawaheshimiwi sana sana, ama kuthaminiwa, au hata kupendwa. Wakati mwingine ni kwa sababu ya kutokuwa na unyenyekevu na neema ambayo huo ujumbe umewasilishwa.. Sisi tuna mazoea ya kuwakataa watu wanaonekana kama wenye kiburi ama ubinafsi ama wale wana tabia ya kudunisha wengine kwa sababu tu hawakupata jawabu iliyo sahihi.

Tunapoelekeza wengine kwa Kristo na katika maisha ni muhimu kutoenekana kama tuna majivuno ama tumejiinua. Ni Mungu mwenyewe anayeshiriki hekima Yake na sisi ili kwa unyenyekevu na neema bila hatia tushiriki na watu wengine. Kuwa na ujasiri na ushupavu lakini usikuwe na madharau.

*Ombi la leo*

Baba, nakuomba leo unipe roho wa unyenyekevu, na ujasiri na ushunjaa. Nisaidie nione wengine kama ninavyotaka wanione. Wacha sheria ya huruma iwe kwa ulimi wangu ninapo onyesha wengine njia Yako na masikio yangu pia yawe wazi kwa ushauri Wako kupitia wengine.

*Maandiko ya leo*

Yakobo 3:2 Lakini kama mtu hakosi katika usemi wake, basi, huyo ni mkamilifu, na anaweza kutawala nafsi yake yote.

1 Petero 5:5 Kadha\’lika nanyi vijana mnapaswa kujiweka chini ya mamlaka ya wazee. Ninyi nyote mnapaswa kuwa na unyenyekevu mpate kutumikiana; maana Maandiko Matakatifu yasema: "Mungu huwapinga wenye majivuno, lakini huwajalia neema wanyenyekevu."

Waebrania 10:35; Basi, msipoteze uhodari wenu, maana utawapatieni tuzo kubwa.

## *Yafaa mtu ajaribiwe katika pahali pa siri pa maisha kabla ainuliwe hadharani maishani*

Bibilia inasema jinsi tulivyo waaminifu kwa mambo madogo, basi Mungu atatupa mambo makubwa tusimamie. Hata hivyo, wakati mwingine huonekana kama hatufanyi maendeleo yoyote. Yususfu alielewa kanuni hii na akaendelea kuwa mwaminifu hata wakati ilikaa ni kama Mungu

amemwachilia. Safari yake kuelekea siku kuu yake ilimpeleka kwa shimo na gereza kabla afike ikulu. Ni ndani ya shimo na gereza ndipo Yusufu alijaribiwa kwa pahali pake pa siri kwa maisha yake kabla ainuliwe hadharani maishani mwake.

Kumbuka kuwa wakati mwingine lazima tuachilie ili tuinuliwe na mara nyingi kile tunachangwa moto tuachilie ni nia yetu na itikadi za maisha zinazoweza kuturudisha nyuma tusifikie ubora wa Mungu. Usinung'unikie changa moto zile za maisha zinazokusukuma karibu na Mungu.

*Ombi la leo*

Baba, naomba unisaidie kuwa mwaminifu kwa majukumu madogo Unayonipa. Nikumbushe kusoma Bibilia, kuomba bila kukoma, kukuabudu kila siku, na kushiriki imani yangu. Nitakuwa na uendelevu, bila kuangalia hali za maisha. Niondelee zile vitu zinazozuia mbio zangu.

*Maandiko ya leo*

Mathayo Mtakatifu 25:2 Watano miongoni mwao walikuwa wapumbavu na watano walikuwa wenye busara.

Warumi 12:2 Msiige mitindo ya ulimwengu huu, bali Mungu afanye mabadiliko ndani yenu kwa kuzigeuza fikira zenu. Hapo ndipo mtakapoweza kuyajua mapenzi ya Mungu, kutambua jambo lililo jema, linalompendeza na kamilifu.

## ***Mungu hajakwama kwa siku zako zilizopita***

Je, unajua Mungu hata hakumbuki siku zako zilizopita? Sio dhambi zako tu na upungufu, lakini anaamua kutokumbuka mahali ulikosea huko nyuma pia… sehemu za maisha yako unazowazia zinaongeza ama kupunguza udhamana wako wa kibinafsi, heshima ambazo zilikupita, kupandishwa cheo ulikokosa kupokea na wakati umenoa mtihani wa maisha.

Mungu natamani sana siku zako za usoni. Kuna sababu kioo cha mbele cha gari ni kikubwa kuliko cha nyuma. Tazamia usoni mwako na Bwana na uache mambo yaliyopita nyuma. Mpango wa Mungu kwa maisha yako bado uko mbele na hajakwama kwa siku zako zilizopita.

*Ombi la leo*

Baba, ahsante kwa siku zangu zilizopita. Nisaidie nijifunze kutokana na yote niliyokutana nayo maishani mwangu. Nitachunguza makosa yangu nikiangalia usoni mwangu na Wewe. Najua mawazo uliyo nayo kwangu, mawazo ya siku bora na tumaini. Tumaini la kesho bora. Nakushukuru mbele kwa siku zangu mkuu za usoni!

*Maandiko ya leo*

Micah 7:9; atarejea na kutuhurumia; atayakanyaga maovu yetu; nawe utazitupa dhambi zote zao katika viridi vya bahari.

Yeremia 29:11; maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani wala sio ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho

Zaburi 103:12 kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi.

Warumi 8:12 Lakini ninyi hamuishi kufuatana na matakwa ya mwili, bali kufuatana na matakwa ya Roho, ikiwa Roho wa Mungu anaishi ndani yenu. Yeyote asiye na Roho wa Kristo, huyo si wake Kristo.

## *Kila unachotaka chaweza kukugharimu kila kitu ulicho nacho*

Bibilia inasema hadithi ya mtu aliyepata mlango wa mgodi uliokuwa umefichwa shambani. Alifurahi sana hata akauza yote aliyokuwa nayo apate kununua hilo shamba. Hivyo ndivyo alivyoidhamini hazina hiyo. Yesu akasema hivi ndivyo kuwa mkristo inafaa kumaanisha kwetu sisi.(mathayo Mtakatifu 13:44). Wacha tupate jawabu lile kupitia swali lingine.

Unawazia nini kuhusu mtu ambaye muumbaji wa dunia, ambaye angepata yote atakayo alilipa gharama kubwa zaidi ya mawazo yetu akitarajia kuanza uhusiano na yule mtu? Huyu mtu anaonekana kama ni hazina spesheli… na ni kweli. Kama yule mtu katika hadithi ya Yesu, Mungu alitoa kile bora zaidi alikuwa nacho, alitoa yote aliyokuwa nayo-kwa fursa yaku “chimba” uhusiano na wewe. Kwa maana Mungu anakupenda kiasi hicho, inafaa kumpenda na kumdhamini pia. Ni gharama gani unayoweza kulipa ili kuanza uhusiano na Mungu?

*Ombi la leo*

Baba, ahsante kwa kunipenda kiasi kikubwa. Nifanye nini kusema "ahsante" kwa yote uliyonitendea? Tafadhali dhihirisha upendo Wako kwangu na unionyeshe udhamana wangu katika macho Yako. Nina nyenyekezwa na ninashukuru kwa upendo Wako.

*Maandiko ya leo*

Luka Mtakatifu12:34 Pale ilipo hazina yako, ndipo pia utakapokuwa moyo wako.

1 Yohana 4:19 Sisi tuna upendo kwa sababu Mungu alitupenda kwanza.

## ***Unawazia nini kuhusu huyu mtu ambaye muumba wa dunia yote, ambaye angepata chochote akitaka, alilipa gharama ya juu inayoweza kuwaziwaa akitarajia ataweza kuwa na uhusiano na huyu mtu***

Udhamana wa kitu sanasana hudhihirishwa na kile mtu ako tayari kulipa kwa sababu ya hicho kitu. Mungu alimpenda mwanadamu sana kwamba alikubali kumtoa Mwanaye juu ya msalaba wa Karivali ili apate nafasi ya kuanza uhusiano na wewe. Alinunua fursa hiyo na anatamani kumfanya kila mtu mtoto Wake.

Tunapo wapita watu mitaani, sokoni, ama kwa sehemu za starehe, twafaa kujua udhamana wa kila mmoja wao ni kama ya mwana wa Mungu katika macho ya Baba na tunafaa kuchukuana mmoja kwa mwingine jinsi Mungu anavyotuchukua sisi. Kwa sababu ya Kristo twafaa kuangalia kila mmoja bila kujalisha kabila, jinsia, alipozaliwa, ama hali yake ya uchumi kama Mungu anavyotuuchukulia sisi.

*Ombi la leo*

Bwana, nahitaji msaada wako kuwaona watu wote kama wale wamepewa uhai wa Mwanao Yesu Kristo uwafikie. Nisaidie niwakumbatie kama wewe na niwe tayari kuwafanya sehemu ya jamii yangu ya kiroho kama ndugu na dada katika Kristo. Nisamehe mahali nimewaonea wengine na unisafishe. Amina.

*Maandiko ya leo*

Waefeso 4:32 ;Muwe na moyo mwema na wenye kuhurumiana; kila mmoja na amsamehe mwenzake kama naye Mungu alivyowasamehe ninyi kwa njia ya Kristo.

Yohana 13:34; Nawapeni amri mpya: pendaneni; pendaneni kama nilivyowapenda ninyi.

1 Yohana 4:7-8; Basi, mwanamke mmoja Msamaria akafika kuteka maji. Yesu akamwambia, "Nipatie maji ninywe." (Wakati huo wanafunzi wake walikuwa wamekwenda mjini kununua chakula.)

Matendo ya Mitume 10:34 ;Hapo Petro akaanza kusema: "Sasa nimetambua kwamba hakika Mungu hana ubaguzi.

## ***Kutowachilia jambo kuu kwa ushauri kwa kuogopa ushauri wa mungu waweza kuwa kinyume na jambo hili ni kutenda kama mpumbavu na kushirikiana na udanganyifu.***

"Kukana kutojua" inaelezea hali ambapo mtu anakataa maneno yenye kumpea ufahamu Fulani wa mambo anayokisia yako kwa sababu ya manufaa yake ya "kutojua". Kisheria, mawakili wanaweza kutumia mbinu hii kukwepa kutozingatia maadiri ya kiuanadamu. Katika siasa, wenye kuhusika waweza kutumia haya kukwepa kushikamana na mambo wanayounga mkono, na ndani ya nyumba yako mtoto aweza kuitumia ili asiadhibiwe kwa makosa ambayo amejiletea mwenyewe- "lakini mimi sikujua."

Ukweli wa mambo ni kwamba sisi sanasana hujua wakati kitu ambacho tunafikiria ama tunapanga ni makosa hata kabla hatujakitenda. Neno la Mungu linatuambia kwamba Roho Mtakatifu hutuonyesha makosa yetu, na huwaelekeza watoto wake kwa ukweli ( Yohana Mtakatifu 15:8,13). Kutowachilia jambo kuu kwa washauri kwa kuhofia kwamba ushauri wa kiungu utakuwa kinyume ni kutenda kama mpumbavu na kushirikiana na undanganyifu. Hiyo ni karibu sana na kusema, " najua hii ni makosa, lakini ninatenda hata hivyo." Na hapo ni pahali hatari kuwa.

*Ombi la leo*

Mungu, nataka kukupendeza Bwana. Wakati mwingine ni mng'ang'ano wa ukweli kuambatanisha mipango yangu na kile ninafikiria unataka. Tafadhali ninenee kwa njia wazi, na unionyeshe jinsi ya kushirikiana na wewe na unipe washauri wazuri wa kiungu.

*Masomo ya leo*

Mithali 18:1; mtu anayejitenga anatafuta mapenzi yake mwenyewe; anapingana na uamuzi wote wa hekima.

Yohana Mtakatifu 3:20-21; Kila mtu atendaye maovu anauchukia mwanga, wala haji kwenye mwanga, maana hapendi matendo yake maovu yamulikwe. Lakini mwenye kuuzingatia ukweli huja kwenye mwanga, ili matendo yake yaonekane yametendwa kwa kumtii Mungu."

## ***Wakati Mwingine Mungu anatarajia tujaribu yasiyowezekana.***

Neno la Mungu limejaa watu ambao walichangwa moto kujaribu mambo yasiyowezekana. Hadithi kama hiyo inamuhusisha kilema aliyeitwa Namani. Alichangwa moto na nabii Elisha ajirushe mara saba mto Yorodani ili ukoma uishe na hivyo aponywe naye Mungu. Namani alijawa na maswali mengi kulingana na mwelekeo huu ulionekana kama usiowezekana na usio wa kawaida. Hata hivyo, Namani alitiwa moyo na rafiki yake kujaribu yasiyowezekana kwa vile ni nabii wake Mungu alikuwa amenena. Matokeo ya utiifu wa Namani ilikuwa uponyaji.

Hata sisi lazima wakati mwingine, tushughulikie changa moto za maisha kwa kujaribu yasiyowezekana kwa vile tumelipokea neno la Mungu.

*Ombi la leo*

Baba Mungu, ninenee na uniongoze kwa Njia Yako kwa maisha yangu. Nipe neema ya kujua sauti yako na unitie moyo kujaribu hata yale yasiyo wezekana Unapo nielekeza. Pia, Baba, niwezeshe kuwatia moyo wale wengine wakuamini zaidi katika hali zao na wakauamini kuzidi uweza wao.

*Maandiko ya leo*

2 wafalme 5:13-14; na watumishi wake wakaja nakumnenea wakisema, “ baba yangu, kama nabii angekuambia ufanye jambo kubwa, je, haugefanya? Ni lipi zaidi, anapokuambia, “oga, na uwe msafi?” kwa hivyo akateremka chin ina kujirusha ndani mara saba mto Yorodani, kulingana na msemo wa mtu wa Mungu; na mwili wake ukarejeshwa kama wa mtoto, na akawa msafi.

Mathayo Mtakatifu 19:26; Yesu akawatazama, akasema, "Kwa binadamu jambo hili haliwezekani, lakini kwa Mungu mambo yote huwezekana."

Marko Mtakatifu 9:23; Yesu akamwambia, "Eti ikiwa waweza! Mambo yote yanawezekana kwa mtu aliye na imani."

## ***Usalama wako wa kibinafsi na usawa wako labda hazikuwa mtazamo wa kimsingi wake Mungu aliposema, “Enendeni mkafanye wafuasi”***

Wakristo wengi duniani wanafahamu “theolojia ya Ndoto ya Marekani.” Theolojia ya Ndoto ya Marekani huyachambua maandiko kuonyesha kwamba waumini wote wametunukiWa na Mwokozi wao haki Fulani, kama maisha, uhuru, na kutafuta furaha. Maandiko hata hivyo, huelezea “theolojia ya Kifalme” kama ile ina gharimu tujikane, tuchukue msalaba na tumfuate Yesu.

Ingawa Mungu kwa hakika anatamani na anahusika na afya yako na ubora wako, labda sio shabaha Lake la kimsingi anapoona kuwa watu bado wamepotea, wanakufa, na wanaenda jehanamu. Lazima, basi tugundue mapenzi ya Bwana kuhusu maisha yetu kwa njia ya upana kuliko vile inatuhusu sisi binafsi na ndoto zetu za kufanikiwa.

*<u>Ombi la leo</u>*

Bwana, hii ni dunia Yako, sio yangu. Wakati mwingine ninasahau kwamba maisha sio kuhusu mimi binafsi. Tafadhali badilisha roho yangu ili nipende vitu unavyovipenda, nifurahishwe na vile vinavyokufurahisha. Najua kuna watu “wenye njaa” pahali kwingine. Nionyeshe jinsi ninavyoweza kufanya sehemu yangu kushiriki pamoja nao.

*<u>Maandiko ya leo</u>*

Mathayo Mtakatifu 16:24; Kisha Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Kama mtu yeyote anataka kuwa mfuasi wangu, ni lazima ajikane mwenyewe, auchukue msalaba wake, anifuate.

Zaburi 46:10; nitainuliwa juu ya mataifa, nitaheshimiwa dunia nzima.

Mathayo Mtakatifu 6:10 Ufalme wako ufike. Utakalo lifanyike duniani kama mbinguni.

## ***Neno la Mungu hutueleza yote yenye Mungu amekwisha fanya na yale Atafanya***

Kama yote tunayotenda ni kusoma Bibilia, basi yote tunayoweza kuona ni yale Mungu ameshafanya. Bibilia, ikitazamwa kama tu historia, hudhihirisha mahali Mungu ameshakuwa, yale ameshafanya, na jinsi aliyafanya.  Hata hivyo Bibilia ni zaidi ya historia…ni agano linaloishi, sio la vile tu Mungu alifanya lakini pia ya vile atakavyofanya. Mungu ni yule jana, leo na hata milele. Anza kusoma Neno la Mungu ujue yote aliyoyafanya na anayotaka kuyafanya sasa. Mungu anataka kufanya nini? Yale yale ameshafanya awali.

Mungu anataka watu wasikie injili, alete uponyaji kwa waliovunjikiwa, aweke mateka huru, arejeshe macho kwa vipofu, akomboe wale ambao wamefinyiliwa chini na atangaze siku kuu ya Bwana, anataka kutenda haya kupitia kwako wewe.

*Ombi la leo*

Mungu, nataka kukujua Wewe. Nataka kuwa pahali ulipo na nataka niungane na Wewe kwa yale uyatendayo. Naomba utajidhihirisha kwangu na unionyeshe jinsi ninavyoweza kukujua vizuri leo kuliko nilivyokujua jana? Tafadhali nipe macho yanoyokuona Wewe, masikio yanayo kusikia Wewe, mikono inayokushika Wewe, na miguu inayokufuata Wewe.

*Maandiko ya leo*

Waebrania 13:8 Yesu Kristo ni yuleyule, jana, leo na milele.

Luka Mtakatifu 4:18-19; "Roho wa Bwana yu juu yangu, kwani amenipaka mafuta niwahubirie maskini Habari Njema. Amenituma niwatangazie mateka watapata uhuru, vipofu watapata kuona tena; amenituma niwakomboe wanaoonewa, na kutangaza mwaka wa neema ya Bwana."

## *Kanisa limeundwa liwe kikosi cha kufanya kazi nacho lakini sio uwanja wa kufanyia kazi*

Kanisa la faa kukua lifanyike jeshi sio la kusikiza tu, kikundi cha washirika ambacho kimepangwa badala ya kuwa watazamaji, mtego unaotumiwa kuwashika samaki badala ya kuwa samaki ambazo kila mara ziko tayari kushikwa. Kwa maneno mengine kanisa ina faa kuwa kikosi cha kufanya kazi nacho badala ya uwanja wa kufanyia kazi.

Wewe ni aina ya mkristo anayehudhuria kanisa kwa kile mchungaji na kanisa waweza kukufanyia ama unahudhulia kanisa kwa kile unaweza kufanyia watu wengine?  Kubali kukomaa na ukumbatia njia komavu

kuhusu kanisa ni nini. Jiwachilie na utazamie kujihami kufanya huduma na utie nguvu mwili wa Kristo.

*Ombi la leo*

Mungu, ahsante kwa kuniokoa! Ahsante kwa kunihusisha na mpango Wako. Najua kuwa mipango Yako ni mikubwa kuniliko mimi, na kwamba una watoto wengine mahali kwingine. Tafadhali nisaidie kukumbuka kwamba Umeniita kuwa mhusika na sio mtazamaji tu.

*Maandiko ya leo*

Waefeso 4:11-15; Ndiye aliyewapa watu zawadi: wengine aliwajalia wawe mitume, wengine manabii, wengine wawe waeneza Habari Njema, wengine wachungaji na walimu. Alifanya hivyo apate kuwatayarisha watu wote wa Mungu kwa ajili ya kazi ya huduma ya Kikristo ili kuujenga mwili wa Kristo, na hivyo sote tuufikie umoja wa imani na kumjua Mwana wa Mungu; tuwe watu waliokomaa na kuufikia utimilifu wake Kristo mwenyewe. Basi, hatutakuwa tena kama watoto, tukitupwa na kupeperushwa huko na huko kwa kila upepo wa mafundisho wanayozua watu wadanganyifu, ili wawapotoshe wengine kwa hila. Ila, sisi tukisema ukweli kwa moyo wa mapendo tutakua zidi katika kila jambo kulingana na Kristo ambaye ndiye kichwa;

## *Kila ujumbe unafaa kuwa jambo ambalo wasikilizaji wanaweza kubeba na kushiriki na wengine*

Kwa kawaida, tunapoenda sokoni kununua bidhaa za kutumia siku zingine tunaziweka ndani ya chombo, kilicho na vishikio, ili tufanye vyombo vyetu vya dhamana kuwa salama salimini na zibebeke kwa urahisi. Ni hivyo na Neno la Mungu. Kupanga Neno la Mungu kwa njia ambayo ni rahisi kukumbuka na rahisi kubeba itatusaidia katika njia za maisha.

Tunapochukua wakati kufunza watu kanuni za Neno la Mungu na watu wanapopeana wakati wao wasikie ni nini unasema, ni muhimu kuweka ujumbe wako na njia ambayo watabeba nyumbani kwa urahisi. Kila ujumbe wa faa kuwa kitu ambacho yule anayesikiliza aweza kubeba na kushiriki na watu wengine.

*Ombi la leo*

Baba, ahsante kwa Neno Lako; naomba unipe kuelewa kwa undani kila siku. Nisaidie kuwa mtendaji wa Neno, na sio msikizi pekee. Na, Baba weka mtu maishani mwangu ambaye ninaweza kupea ujumbe Wako. Nipe maneno Yako ya Hekima ninaposhiriki na wengine.

*Maandiko ya leo*

2 Timotheo 2:2; Chukua yale mafundisho uliyonisikia nikitangaza mbele ya mashahidi wengi, uyakabidhi kwa watu wanaoaminika, ambao wataweza kuwafundisha wengine pia.

Yakobo 1:25; Lakini mtu anayeangalia kwa makini sheria kamilifu ambayo huwapa watu uhuru, mtu anayeendelea kuizingatia, na si kuisikia tu na kuisahau baadaye, bali anaitekeleza, mtu huyo atabarikiwa katika kila kitu anachofanya.

## *Mungu hakupeana mtoto Wake wa ziada ila mtoto Wake wa pekee*

Katika wakati wa agano la kale, dhambi za watu wa Mungu zingesamehewa kama bei ingelipwa. Damu ya mnyama ilifaa kumwagwa, na dhabihu hii ya kujitolea ilifaa kutendwa mara nyingi. Mungu alitamani kuleta njia bora zaidi kwa watu Wake na kwa wao kuwa na msamaha wa umilele. Haya, alisema, hayangetendwa kwa damu ya ng'ombe na mbuzi. Iligharimu damu ya Mwanawe wa kipekee na sasa tuko salama milele.

Mungu hakumtoa mwanaye wa ziada ila wa kipekee.ilimgharimu Mungu kile Chake bora zaidi; hakukuwa na njia nyingine. Kwa vile Mungu hakumjali mtoto Wake wa kipekee kabla yetu, na tumpe kilicho bora zaidi kwetu sisi.

*Ombi la leo*

Baba, namkubali Yesu kama dhabihu ya tosha kwa dhambi zangu. Naamini kuwa damu yake inatuunganisha na Wewe na agano la milele. Ahsante kwa kunipea kile bora sana Kwako- Mwanao wa pekee. Ahsante kwa uzima mpya ndani ya Kristo. Nisaidie niishi kila siku na heshima kwa gharama Uliolipa kwa wokovu wangu.

*Maandiko ya leo*

Yohana Mtakatifu 3;16; Maana Mungu aliupenda ulimwengu hivi hata akamtoa Mwana wake wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

1 Wakorinitho 6:19-20; Je, hamjui kwamba miili yenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, ambaye mlimpokea kutoka kwa Mungu? Ninyi basi, si mali yenu wenyewe. Mlinunuliwa kwa bei kubwa. Kwa hiyo, itumieni miili yenu kwa ajili ya kumtukuza Mungu.

## *Ilimgharimu Mariamu mwanawe wa kwanza ili Mungu aukomboe ulimwengu*

Mungu anapofanya mambo, mara nyingi huhusisha watu. Pamoja na mpango Wake wa maisha yetu zinakuja nafasi zetu za kuhusika. Tunajua na kuamini kwamba wokovu kupitia Yesu Kristo ni huru kwetu, sababu ni kwamba wengine walilipia gharama.

Tangu siku Yesu alituacha na Mwito Mkuu, wamishenari, wahubiri na waijilisti wamewacha kazi zao, starehe za nyumba zao na hata maisha yao wenyewe kuleta injili kwa mataifa. Musa alikuwa na kazi ngumu yakutenda wakati Mungu aliwaweka huru Waisiraeli kutoka Misiri. Esta alikuwa na jukumu hatari wakati Mungu aliwaokoa wayahudi kutokana na kifo. Ilimgharimu Mariamu mwanaye wa kwanza ili Mungu aokoe ulimwengu. Itakugharimu nini wewe ili Mungu atimilize mpango Wake katika maisha yako?  Utakubali kusame “ndiyo”, sio mapenzi yangu ila Yake yafanyike?

*Ombi la leo*

Baba, nagundua ulilipa gharama yangu, na maisha yangu ni Yako sasa. Ahsante kwa kuwa na mpango mzuri wa maisha yangu. Naomba ufanye mawazo yangu yakubaliane na mawazo Yako na unionyeshe sehemu yangu katika mpango Wako mkuu. Nisaidie niwe mtiifu. Najua kwamba naweza kufanya mambo yote kupitia kwa Kristo anitiiaye nguvu.

*Maandiko ya leo*

Mathayo mtakatifu 16:24; Kisha Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Kama mtu yeyote anataka kuwa mfuasi wangu, ni lazima ajikane mwenyewe, auchukue msalaba wake, anifuate.

Luka Mtakatifu 1:38; Maria akasema, "Mimi ni mtumishi wa Bwana, nitendewe kama ulivyosema." Kisha yule malaika akaenda zake.

## *Mungu anasifa ambayo ni ngumu kutikisa*

Mungu ana sifa ya kuwa Mungu mwema, Mungu wa upendo, Mungu mwenye upole na huruma, mwenye kuaminika na wa ukweli. Pia Mungu

ana historia ya kuwa imara dhidi ya maadui Wake, aliyemaanisha kuhusu dhambi, na ambaye amejitolea kushinda kila vita. Kwa maneno mengine, Mungu anaweza kuaminiwa kuwa Mungu na hivyo ndivyo amekuwa wakati wote na atadumu hivyo. Ana sifa ambayo ni ngumu kutikisa.

Nabii Malaki alitangaza, “Mimi ni Bwana Mungu, sibadiliki.” Tunaweza kuamini kwamba Mungu ataendelea kuwa kile tumemuona kila siku akiwa. Anayekupenda na aliyetoa Mwanaye kwa sababu yako na hatakuwacha na hata kutupilia. Mungu ni mzuri.

*Ombi la leo*

Bwana, Mungu wa mbinguni, Wewe ni mkuu na wakupendeza. Wewe kwa njia ya kuaminika unaweka ahadi zako kwa yeyote anayekupenda na kutii amri Zako. Naomba ukumbuke ahadi ulizofanya. Ulisema dhambi zetu zinaweza kututenganisha na Wewe. Kisha pia ukasema bila kujalisha tumekiuka kiasi gani, tukikiri dhambi zetu na tukutii Wewe, Utatusamehea na uturejeshe kwa uhusiano sawa na Wewe.

*Maandiko ya leo*

Hesabu 23:9, ‘Mungu sio mwanadamu, ili andanganye, wala sio mwana wa mtu , ili Atubu. Amesema na hatatenda? Ama amenena na hatafanya itimilike?

Zaburi 89:34; agano Langu, sitalivunja, na wala sitabadilisha neno ambalo limetoka kwa kinywa changu.

Yakobo 1:17; Kila kipaji chema na kila zawadi kamilifu hutoka mbinguni; hutoka kwa Baba, Muumba wa mianga, ambaye habadiliki wala hana alama yoyote ya ugeugeu.

## ***Unachofanya unapo mngojea Mungu kitabainisha utangoja kwa muda kiasi gani***

Daudi alijua kumngonjea Mungu kuna maanisha nini. Alifanyika masihi wa Kifalme akiwa miaka kumi na sita, wala hakufanyika mfalme hadi akafikisha miaka thelathini. Yaweza kaa ni kama Mungu hajibu maombi yetu ama haelewi uharaka wa hali yetu. Mawazo yanamna hiyo huonyesha Mungu hayuko kwa usukani. La kweli ni kuwa Mungu sanasana hutumia kungonjea kutuhuisha, kutufanya wapya, nakutuandaa kwa siku kuu yetu. Tuna weza tumia wakati wetu vizuri tukiweka kina na kutia nguvu uhusiano wetu na Mungu uandalizi wetu kufanya mapenzi Yake.

Kile unachofanya wakati unamngojea Mungu kitabainisha utamngojea muda kiasi gani. kuwa na mazao. Fanya jambo lenye maana ukiwa bado uko na wakati.

*Ombi la leo*

Nitakungojea Wewe.. kwa maana Wewe unafaa kungojewa. Ahsante kwa kuniweka na amani wakati mawazo yangu yanakuelekea Wewe. Mapenzi ya nafsi yangu ni Kwako. Wewe ni mwamba wangu na wokovu wangu, tarajio langu ni kwako. Nitaendelea kujifunza subira na haki hadi unudhihirishie kusudi Lako timilifu kwangu kwa mambo yote.

*Maandiko ya leo*

Zaburi 40:11 nilimngojea Bwana kwa subira, akaniinamia akakisikia kilio changu akanipandisha toka shimo la uharibifu, toka undongo wa utelezi; akaisimamisha miguu yangu mwambani, akaziimarisha hatua zangu.akatia wimbo mpya kinywani mwangu, ndiyo sifa zake Mungu wetu; wengi wataona na kuogopa nao watamtumaini Bwana.

## *Wakati mwingine nchi ya ahadi siyo ile tuliyoahidiwa bado*

Wana wa Isiraeli waliambiwa na Musa kwamba Mungu alikuwa akiwatoa kwa utumwa wa Misiri hadi nchi ya maziwa na asali. Waliambiwa hii nchi ya ahadi ya kanani ingekuwa pahali ambapo wangekula bila kukosa, wakunywe kutoka kwa visima ambavyo hawakuchimba, hawangekosa chema chochote na wapumzike kutoka kwa maadui wao wote. Hata hivyo, walipoingia nchi ya ahadi walikuta sio vile waliambiwa.

Nchi ya Kanani ilikuwa na uwezo wote ambao Musa alikuwa ametangaza, lakini kwa sasa, ilikuwa uwanja wenye maadui ambao wangeshindwa kupitia vita ambavyo lazima zingepiganwa. Walipohusika na Mungu, yale Mungu alikuwa ameahidi, alifanya. Hata hivyo, hakufanya bila msaada wao. Kama kile Mungu amekuahidi sio kile amekuahidi bado, endelea kufanya kazi na yeye na ataweka ahadi Yake.

*Ombi la leo*

Baba, nanyenyekea kwa mpango Wako kwa maisha yangu na naungama kufanya kazi na Wewe kufanya ndoto zako kutimia. Nionyeshe, ewe Bwana jinsi ya kuvumilia na kuendelea bila kukoma ninapojifinyilia katika ahadi Zako kuhusu maisha yangu. Ahsante Bwana. Amina.

*Maandiko ya leo*

Mathayo Mtakatifu 11:12; Tangu wakati wa Yohane mbatizaji mpaka leo hii, Ufalme wa mbinguni unashambuliwa vikali, na watu wakali wanajaribu kuunyakua kwa nguvu.

Warumi 4:21; Alijua kwamba Mungu anaweza kuyatekeleza yale aliyoahidi.

## *Tunachofanya na kile tulicho nacho kitabainisha tutakachopata*

Fumbo la Yesu la talanta inafanya tugundue kwamba baraka na uwezo wetu ni vipawa kutoka kwa Mungu na zinakuja na wajibu wa utumishi. Hii inaitwa utumishi na hailinganishwi na pesa pekee lakini pia na karama yetu, pesa, na shani zingine. Utumishi ni kuangalia vipawa ambavyo Mungu ametuaminia sisi. Mungu sio rahisi akupe kile hawezi peana kupitia kwako wewe.

Fumbo la talanta, utumishi mzuri, na kuwa mwaminifu kwa mambo yaw engine yanalenga ukweli kwamba Mungu anatutarajia tuwe waaminifu na watumishi wenye hekima na tutumie baraka zetu kufanyika baraka kwa watu wengine. Ni nini uko nacho ambacho Mungu anaweza kutumia kuimarisha Ufalme Wake duniani. Kile utafanya na kile ulicho nacho, kitabainisha ni nini zaidi utakachopata cha kufanya kazi nacho.

*Ombi la leo*

Mpenzi Bwana, ahsante kwa kuniaminia shani zote zinazonibariki na kuniwezesha kubariki wengine. Jinsi nilivyo muaminifu, niongeze, Bwana, ili nifanye zaidi kwa ajili Yako.

*Maandiko ya leo*

Luka Mtakatifu 19:17; Naye akamwambia: `Vema; wewe ni mtumishi mwema. Kwa kuwa umekuwa mwaminifu katika jambo dogo, utakuwa na madaraka juu ya miji kumi!`

Luka Mtakatifu 16:10; Yeyote aliye mwaminifu katika mambo madogo, atakuwa mwaminifu katika mambo makubwa; na yeyote asiye mwaminifu katika mambo madogo, hatakuwa mwaminifu katika mambo makubwa.

## *Mungu hatengenezi viongozi, niwatumishi pekee...watumishi hutengeneza viongozi*

Wazia ukitumia maisha yako yote ukipanda ngazi, kisha ugundue kumbe ngazi hiyo iliegemea jengo lisilofaa. Tunaelezwa kuwa watu wengi hutumia nafasi ya kwanza ya maisha yao wakitafuta fanaka na ya pili wakitafuta umuhimu. Watu wengi wanataka kuwa wakuu kwa macho ya mtu fulani…ni kwa macho ya nani utakuwa mkuu? Wakati dunia nzima inatafuta viongozi, Mungu anatafuta watumishi.

Ukitaka kuwa mkuu kwa ufalme wa Mungu, lazima ufanyike mtumishi kwa wote. Kwa yule anayetaka kuwa chifu kati yenu lazima afanyike mtumishi wa wote. Yesu alikuja kutumika, sio kutumikiwa. Hauwezi kufanya bora zaidi.

*Ombi la leo*

Baba, ahsante kwa kutupea Yesu awe kielelezo kikamilifu. Nisaidie nifanyike mtumishi kwa wale wote ninaowapenda na wale unanipa fursa ya kupenda. Nataka kuwaongoza watu kwa kuwatumika.

*Maandiko ya leo*

Marko mtakatifu 10:45; Maana Mwana wa Mtu hakuja kutumikiwa, ila alikuja kutumikia, na kutoa maisha yake kuwa fidia ya watu wengi."

Wafilipi 2:5; wacha nia hii iwe nanyi ambayo ilikuwa pia na Kristo Yesu

Marko mtakatifu 10:44; Anayetaka kuwa wa kwanza, sharti awe mtumishi wa wote.

## *Ukweli usio na kujukumika huumiza wengine hata wakati ni sahihi*

Umekuwa ukiongeza uzani? Labda ni mavazi. Unaonekana umenona. Aah… huo ndio ukweli.

Mara nyingi tunapata fursa ya kusema maneno ambayo yanaweza kuumiza moyo, kukwaza, ama yakujipenda wakati hakuna faida zaidi ya tamko lisilo kuwa limewaziwa. Sanasana, watu ambao hunena zaidi huumiza watu wengine huku wakijitetea kwa msemo kuwa, “ aah, ni ukweli.” Kwamba tu kitu ni ukweli haikupei haki ya kukisema bila kutafakari madhara yake kwa wengine. Bibilia inatukanya tusiwaumize wengine na maneno yetu ama msemo wetu wenye kukasirisha pasipo na faida ya Kiufalme.

*Ombi la leo*

Mungu, na nyenyekeza mawazo yangu na maneno ya kinywa changu kwa uhifadhi Wako. Nakuomba ulinde mdomo wangu na ulimi wangu ili niweze kuleta baraka  na mazungumzo yasiyo msumbua anayesikia maneno yangu. Ahsante Baba.

*Maandiko ya leo*

Yakobo 3:2; Sisi huwatia farasi lijamu kinywani mwao ili watutii; na kwa njia hiyo twaweza kuwaongoza kokote tunakotaka.

Waefeso 4:29; Maneno mabaya hata yasisikike kamwe miongoni mwenu; kila mara maneno yenu yawe ya kufaa na ambayo hujenga na kuwasaidia wengine, ili yawaneemeshe wasikilizaji wenu.

Zaburi 141:3; weka mlizi, Ewe Bwana , kwa kinywa changu;  chunguza milango wa midomo yangu

## ***Hakuna mmoja wetu awezaye mambo yote,lakini kila mmoja wetu anaweza kufanya jambo***

Mungu amelipea kanisa jukumu kubwa- kufanya wanafunzi kwa mataifa yote. Hii inahusisha kuhubiri, kuponya, kufunza, kutoa, kusimamia, kujenga na majukumu mengine mengi. Kama tungekuwa tukutimiza majukumu haya kama watu binafsi, labda tungekata tamaa bila hata kujaribu. Haingewezekana. Lakini Mungu hutuita kama washirika wa mwili Wake ambapo wengine wetu waweza fanya jukumu moja na wengine.

Hatuwezi kufanya mambo yote, lakini kila mmoja wetu anaweza kufanya kitu. Kifunguo cha fanaka katika mwili wa Kristo ni umoja, kila mmoja akitenda jambo na akilitenda kwa kusikilizana.  Pamoja tunaweza kumtumikia kwa njia timilifu kuliko mtu peke yake. Ni mazoea ya wanadamu kuangalia kwa upana kile tunaweza kufanya pekee na kwa njia ndogo yale tunaweza kufanya pamoja. Kama mwili wa Kristo, twaweza kutimiza zaidi tukifanya pamoja kuliko jinsi tunavyoweza hata kuota tukifanya kazi peke yetu. Unganisha maisha yako na nguvu zako kwa wengine ili kazi ifanyike.

*Ombi la leo*

Bwana, nikumbushe kwamba mimi ni sehemu ya mwili Wako hapa duniani hii. Nisaidie kuungana na wale wanao nizunguka kwa njia inayo maanisha. Ahsante kwa kuwaleta watu kwa maisha yangu. Wacha niwe baraka kwa wote ninao watumikia. Ahsante, Bwana, Amina.

*Maandiko ya leo*

Warumi 12:5; Hali kadhalika ingawa sisi ni wengi, tu mwili mmoja kwa kuungana na Kristo, na kila mmoja ni kiungo cha mwenzake.

Muhubiri 4:9; wawili ni wazuri kuliko mmoja, maana wana ujira mzuri wa kazi yao.

Waefeso 4:16; chini ya uongozi wake, viungo vyote vya mwili hushikamana pamoja, na mwili wote hutegemezwa kwa msaada wa viungo vyake. Basi, kila kiungo kikitekeleza kazi yake ipasavyo, mwili wote hukua na kujijenga katika upendo.